

Let's teach each other! This newsletter is published by The Foundation for Tomorrow and is meant to be a venue for teachers and schools to share and learn from each other's best practices.

Issue 6, December 2016

In this issue:

- 4** Life Skills Corner:
Shindano la Uandishi wa Insha na Uchoraji wa Picha
- 6** Educator Innovator: Mbinu ya Jigsaw
- 8** Teacher Talk: Usimamizi Bora wa Darasa
- 9** Psychosocial and Health Corner: Kurejesha Watoto Waishio Mitaani Katika Malezi ya Familia
- 10** In Focus: Cornerstone Leadership Academy



Mwalimu Bora 2016

Wanafunzi wa leo wanakuja shulenii wakiwa na madaftari, kalamu na mabegi yao. Wanafunzi wa leo wanakuja shulenii wakiwa na hamu ya kutaka kujifunza nakuja mambo mengi. Kwasehemu kubwa, wanafunzi wanakuja shulenii wakiwa na lengo lakutaka kujifunza. Lakini kuna wengi wanakuja shulenii wakiwa na changamoto nyingi katika masomo, matatizo ya kinidhamu au maadili, matatizo ya kihisia, matatizo katika familia wanazo toka na mengineyo. Kwa sababu ya changamoto hizi, walimu wanalazimika kufanya kazi za ustawi wajamii, ushauri nasaha na hata pia kuchukua nafasi ya mzazi.



Do you want to be in our next issue?

We want to hear from you! If your school has newsworthy events, projects you are proud of, or thoughts you want to share that would benefit your fellow educators and other school managers, send them to us and we will publish them in the next edition of Tufundishane! Articles that talk about best practices will be given preference, but we also welcome literary contributions such as essays and poems from educators and students.



“Mwalimu bora ni moja kati ya sababu kuu zina muwezesha mwanafunzi kufanya vyema katika masomo na maisha yake kwa ujumla” – Mh. Fabrian Daquro, Mkuu wa Wilaya- Arusha Jiji akikabidhi tuzo kwa walimu bora 2016.

Ni vigumu sana kuwa mwalimu katika shule za leo! Hata kwa waalimu bora inafikia wakati wanachanganyikiwa.

Swali muhimu ni kwamba, nijinsi gani tunaweza kuwahamasisha walimu?

Kama kweli tunataka kufanikiwa kuwahamasisha waalimu waendelee kuwepo mashulenii ni lazima tuanze kuwahamasisha kuanzia mwanzoni mwa muhula mpaka mwisho wa muhula.

Shirika la “The Foundation For Tomorrow” (TFFT) limethubutu kusimama mstari wa mbele ili kuhakikisha linaunganisha walimu waendelee na jitihada za kufundisha watoto mashulenii katika ubora wa hali ya juu.

Shirika la TFFT linatoa fursa za kuhamasisha na kuchochea walimu, kwa kuanda ‘**Tuzo ya Mwalimu Bora**’ (Teacher of Distinction Award) kwa kila mwaka. Kwa mwaka mwingine tena tumeweza kutoa tuzo kwa walimu bora wa Jiji la Arusha na Wilaya ya Meru.

Lengo kuu la tuzo hii ya mwalimu bora ni kutia hamasa, changamoto na motisha kwa walimu wote ili waweze kufundisha watoto wetu kwa ubora zaidi. Ni dhahiri kwamba, mwalimu aliye hamasika, anajithamini na kuithamini kazi yake.

Vilevile anakuwa na mtazamo bora na mwenendo mzuri, wanafunzi na wafanyakazi wenzake hufurahia kujifunza kutoka kwake. Anatumia kipawa chake na marazote


annahakikisha anafanya mambo katika ubora wa hali ya juu. Anakuwa na juhudii, anaipenda kazi yake na pia anastawisha mazingira mazuri kwa wanafunzi kusoma na kujifunza.

Tofauti na kutoa mafunzo kwa walimu, jenzo na zana za kufundishia ni miaka kadhaa sasa shirika la The Foundation For Tomorrow limeendelea kutoa tuzo ya walimu bora kwa waalimu wa halimashauri ya Meru na Jiji la Arusha. Lengo ni ku hakikisha waalimu wanahamasika na wanaweweze; Kujithamini, Kuwa na mtazamo bora kuelekea kazi yao, kukuza au kutumia vipawa vyao katika ubora wa hali ya juu bila kusahahu kuwa na

juhudui kazini.

Zoezi la kuwatafuta waalimu bora mkoaa wa Arusha mwaka wa 2016 lilihusisha halimashauri mbili. Halmashauri ya Jiji la Arusha na Meru. Mchakato wa kuwapata walimu bora mwaka huu ulihusisha usamabazaji wa fomu kwa ajili ya wanafunzi na walimu kuwapendeleza walimu bora kwa mujibu wa vigezo vilivyo bainishwa. Vigezo vilivyo tumika katika mchakato mzima ni pamoja na:

Uwezo wa kuchochaea ufikiri na uchambuzi wa kina mionganii mwa wanafunzi; Uwezo wa kujenga mazingira ya wanafunzi kuhamasika na uzoefu wa kujishughulisha katika kujifunza; Uwezo wa kuwa mvumbuzi katika mbinu za ufundishaji na uendelezaji wa mtaala; Kujitoa kuwasaidia wanafunzi wanao hitaji



msaada katika kujifunza; Haiba/Utu; Ushiriki katika jamii; na Uzoefu katika swala la kufundisha kama mwalimu

Hivyo, kupitia fomu hizo waalimu na wanafunzi kwa kufuata vigezo waliweza kupata nafasi ya kumchagua mwalimu bora.

Kadhalika, mchakato ulihusisha usahili (interviews) na walimu walioshiriki katika tuzo ya walimu bora kutoka katika halmashauri zote mbili. Kwa ushirikiano na wahadhiri wa Chuo Kikuu Cha Arusha-The University of Arusha, kutoka katika kitivo cha elimu, tuliweza kuwafanya usaili na walimu wote walio pendekewa katika swala

zima la kufundisha na kijifunza. Pia wawakilishi kutoka idara ya elimu walikushiriki katika kuwafanya usaili waalimu walio husika.

Vile vile kila mwalimu



alipata muda wa kuandaa somo na kufundisha, zana za kufundishia na kujifunzia, azmio la kazi, andalio la somo pamoja na nukuu za somo. Kwa wastani shughuli zote za ufundishaji kwa kipindi cha miezi sita zilipitiwa.

Mara baada ya kupitia hatua zote tuliweza kupata walimu kumi bora wa mwaka 2016 na hatimaye kufanya sherehe ya kuwapa tuze siku ya mwalimu duniani tarehe 05 Octoba, 2016. Kila mwalimu aliweza kupata cheti cha tuze ya mwalimu bora na kiasi cha fedha laki tano kama tuze. Kwa ushirikiano wa halmashauri ya Jiji la Arusha na Meru, wanataluma na wadau mbalimbali ulimwenguni kote tuliweza kusheherekea kwa pamoja mafanikio na mchango mkubwa wa walimu katika kuelimisha watoto wetu.

Mwisho, nilazima tutambue kwamba licha ya kuwepo majengo, rasilimali mbalimbali, ujuzi na maarifa aliyonayo mwalimu, kama asipo hamasishwa na kushawishiwa kwa



Life Skills Corner

Shindano la Uandishi wa Insha na Uchoraji wa Picha zenyé Ujumbe

Shirika la The Foundation for Tomorrow liliendesha mashindano ya uandisha wa insha na uchoraji wa picha zenyé ujumbe katika shule za msingi za wilaya ya Meru. Shule 52 kutoka kata 21 ziliweza kushiriki. Kila shule shiriki ilipaswa kutoa washindani watatu. Mashindano haya yalihusisha wanafunzi wa darasa la 4-6.

Katika shindano la insha wanafunzi walipaswa kuelezea malengo yao ya baadae, jinsi watakavyofikia hayo malengo, msaada utakaohitajika ili kufikia malengo na vikwazo wanavyodhani vinaweza wakwamisha. Shindano la uchoraji lilihitaji wanafunzi kutumia ubunifu wa uchoraji kuwasilisha mambo anayohitaji motto wa kitanzania kwa maisha mazuri ya baadaye.

Katika uandishi wa insha

wanafunzi walijitahidi, wengi ndoto zao zilikua kuwa waalimu, marubani, madaktari, madereva na raisi. Katika uchoraji tunaona kuna changamoto haswa pale inapompasa mtoto kuweka mawazo yake kwa njia ya picha. Washindi wa uchoraji walijitahidi japo haikuwa kwa kiwango tulichotarajia. Hii inatupatia motisha kuimarisha sanaa na uchoraji shuleni maana ni ajira tosha baadaye.

Zoezi la usahihishaji lilijumuisha jopo la wataalamu wa lugha kutoka chuo kikuu cha Arusha. Walizingatia kanuni na taratibu zote za uandishi na uchoraji pamoja na unadhifu wa kazi kupata

washindi waliopatikana. Tulipata washindi 4 kwa Insha na 3 uchojari. Washindi waliopatikana walipatiwa fedha taslimu na cheti. Shule 10 zilizoongoza pia zilipatiwa cheti kwa ajili ya pongezi. Wafuatao ni washindi na zawaidi walizopata:



Insha

1. Innocent Onesmo-Mbaaseny Maruvango: 200,000

2. Esther Yona -King'ori : 150,000

3. Mercy I Nyiti Mikuuni Malula : 100,000

Continued

4. Anna Swai – Mbaaseny Maruvango :75,000

5. Anna Nassary -Miririny Leguruki : 50,000

Uchoraji

1. Mustafa Matiku- Nambala Kikwe : 200,000
2. Loveness J Akyoo- Shishtony Leguruki : 150,000
3. Ibrahim Eliya - Olkungw'ado Ngarenanyuki : 100,000

Shirika la The Foundation for Tomorrow baada ya mwezi mmoja tulifanya ufwatiliaji kuona zawadi ya fedha taslimu iliwanufaisha washindi kwa kiasi gani. Tulitembelea

wanafunzi watatu walioshinda,

Ester Yona alitumia fedha alizopata kushona nguo za shule, alinunua kuku watatu na fedha nyingine zilitumika kulipa ada ya dada yake anayesoma sekondari ambaye alirudishwa nyumbani kwa kushindwa kulipa ada.

Innocent Onesmo, wazazi wake wamemfungulia account na kumwekea hizo fedha, pia shule ilianaa tafrija fupi kumpongeza yeye na wazazi wake ili kutoa motisha kwa wanafunzi wengine.

Loveness Akyoo alitumia fedha alizopata kushona nguo za shule na kununua viatu, pia alinunua kuku wa kufuga, matumizi kidogo ya

nyumbani na fedha nyingine amekusudia kununua mbuzi. Kwa upande mwingine wazazi wa Loveness wanasema alikua hapendi shule ila kulingana nay eye kutambuliwa kupitia mashindano haya ameahidi kusoma kwa bidii na kuhudhuria shule bila kukosa.

Mashindano haya yalileta picha tofauti kwa shule zilizoshiriki, waalimu wanasema shule za msingi zimesahulika na pia vipaji vyta watoto havitambulikani. Hivyo mashindano haya yametoa mwanga na motisha kwa shule zilizoshiriki. Pia yamesaidia shule zilizoshinda kutambulikana na kuwapatia sifa katika wilaya ya Meru.

Tathmini ya Mradi wa Majaribio wa Somo la Haiba na Michezo (Evaluation of PDS)

Shirika la The Foundation for Tomorrow lilianzisha mradi wa majaribio wa Somo la Haiba na Michezo ambao uliana kutekelezwa mwaka 2015 mwezi wa 4. Mradi huo ulikua na lengo la kuhakikisha wanafunzi wanafundishwa elimu ya stadi za maisha. Waalimu wa somo husika walipatiwa mafunzo na kuhudhuria warsha na

mikutano ili kuboresha ufundishaji wa Haiba.

Shirika lilitoa nyenzo za kufundishia na vitendea kazi pamoja na mtahala uliorahisishwa kufundishia somo la Haiba. Vile vile tumekua tukifwatilia kwa karibu ufundishwaji wa hili somo mashulen (classroom observation). Pia kufwatilia upande wa michezo jinsi wanafunzi wanavyotumia

vifaa walivyopatiwa. Baadhi ya shule ziliweza kushiriki UMITASHUMTA, mfano Sinai Primary kwa sababu ya vifaa tulivyota vyta michezo, vifaa hivyo vilitoa motisha na hari ya kupenda michezo. Shule nyingine zimeanzisha club za michezo zinazohusisha wanafunzi na waalimu, mfano Maua na Upendo shule ya msingi.



Educator Innovator

Mbinu ya Jigsaw

Mbinu ya Jigsaw ni mbinu shirikishi ya kujifunzia ambaye humuweza mwanafunzi kujifunza vyema, inaongeza motisha, na starehe au furaha ya kujifunza. Mbinu hii iligunduliuwa mnamo miaka ya 1970 na Elliot Aronson. Maelfu ya walimu wametumia **jigsaw** kwa mafanikio makubwa kama vile kuongeza matokeo mazuri ya elimu katika ufaulu wa mitihani



Kama ilivyo katika **jigsaw puzzle**, kila kipande in muhimu, kadhalika katika mbinu hii ya kujifunza kila mwanafunzi ni muhimu kwa ajili ya kukamilisha ufahamu kamili wa mada au jambo mwanafuzi analogifunza.

Hatua kumi za kufuata katika utumiaji wa mbinu ya **jigsaw**:

Mbinu ya **jigsaw** ni rahisi sana kutumia darasani, wewe kama mwalimu fuata hatua hizi:

Hatua ya kwanza:

Gawanya wanafunzi katika makundi 5 au 6 ya jigsaw. Kumbuka kuzingatia suala la jinsia, ukabila, rangi, na uwezo katika makundi.

Hatua ya pili:

Teua mwanafunzi mmoja kwa kila kundi kama kiongozi. Kiongozi huyu inatakiwa awe mwanafunzi amabaye anaupo wa kuongoza wenzake katika kundi.

Hatua ya tatu:

Gawanya somo katika vipengele au sehemu 5-6. Mfano, Kama unataka wanafunzi katika somo la historia wajifunze kuhusu Mwalimu Julius K. Nyerere. Unaweza kugawanya wasifu wake katika vipengele vifupi vinavyo jitegemea kama vile; (1) utoto wake, (2) maisha ya familia yake pamoja na mke wake na watoto wao, (3) maisha yake kabla ya kuwa raisi, (4) kazi yake katika lkulu kama kama raisi wa kwanza wa Tanzania, na (5) maisha yake na kazi baada ya kustaafu uraisi.

Hatua ya nne:

Mpe kila mwanafunzi

kujifunza sehemu moja tu. Kuhakikisha wanafunzi wanapata kujifunza sehemu yao wenye tu kulingana na jinsi ulivyo wapa katika makundi.

Hatua ya tano:

Wape wanafunzi muda wa kusoma juu ya sehemu zao angalau mara mbili ili waweze kuelewa vyema. Hakuna haja ya wao kukariri.

Hatua ya sita:

Kwa kila kikundi chagua 'mtaalam' mmoja aweze kuijunga na kikundi kingine ambaye wanakipengele au sehemu sawa zinazo fanana. Wape wanafunzi hawa wataalam muda

wa kujadili pointi kuu ya sehemu zao na wafanye mazoezi ya namna watakavyo onyesha katika makundi yao ya **jigsaw**.

Hatua ya saba:

Warudishe wanafunzi katika makundi yao ya awali ya **jigsaw**.

Hatua ya nane

Mruhusu kila mwanafunzi awasilishe kipengele chake kwenye kikundi. Kuwatia hamasa wengine katika kundi kuuliza maswali kwa ufanuzi.

Hatua ya tisa

Tembelea kila kundi ilikuangalia jinsi wanavyo wasilisha na mwenendo wa mjadala. Kama kuna kikundi chenye matatizo (kwa mfano, mwanafunzi mmoja tu kutawala mjadala au kusumbua), chukua hatua sahihi. Hatimaye, ni vyema

kwa kiongozi wa kikundi kushughulikia swala hili. Viongozi wa vikundi wanaweza kutoa maelekezo kwa kikundi.

Hatua ya kumi:

Mwishoni mwa kipindi toa zoezi kwa wanafunzi kuhusiana na maada au jambo walilokuwa wakijifunza au kujadili na kufanya katika makundi yao. Wanafunzi kwa haraka hutambua kwamba mazungumzo au kazi waliyo kuwa wakiifanya si tu kujifurahisha na kama mchezo lakini ni namna ya kujifunza.

Faida ya mbinu ya jigsaw katika kujifunza

Ikilinganishwa na njia zingine za kufundishia darasani, **jigsaw** kama mbinu shirikishi ya kufundishia ina faida kadhaa:

- Walimu wengi kufurahia

kufundishia mbinu hii

- Ni inaweza kutumika pamoja na mbinu zingine za kufundishia au kujifunzia
- Inaweza tumika hata kwa mda mfupi

Hitimisho

Baadhi ya walimu wanaweza kuhisi kuwa wao tayari wamejaribu kutumia mbinu shirikishi katika madaras yao kwa sababu tu mara kwa mara wamekuwa wakiaweka wanafunzi wao katika makundi madogo na kuwaelekeza washirikiane. Lakini hata hivyo **Jigsaw** kama moja ya mbinu shirikishi za kujifunzia au kufundishia zinahitaji zaidi ya kuwaweka wanafunzi kuzunguka meza na kuwaambia kushiriki, kufanya kazi pamoja, na kupendana au kuwa wa zuri kati ya wao kwa wao.

Continued from page 8...

kufanya vizuri katika masomo.

Jambo ambalo kila mwalimu anatakiwa kujizua asifanye, ni kushiriki au kusababisha mwanafunzi kwa njia yoyote ile achukie kusoma au kujifunza na aache kuhuduria shulen. Elimu ni haki ya msingi ya mtoto ambayo haipaswi

kuingiliwa kwa njia yoyote ile.

Mwalimu anaweza kufundisha, na kurekebisha zaidi küpitia ishara za mwili kuliko hata kuongea. Hii ina pelekea darasa kuwa makini, wanafunzi kuwa wasikiu na mwalimu kuto kengeusha fikra za wanafunzi wengine ambaa ni watulivu. Mwalimu ni mmoja ya wahusika wa darasani kwa hiyo hapaswi

kujifanya yeye ni mtu wapekee kuliko wanafunzi wake.

Pia "utatumia nguvu kidogo na kutokuwa na msongo wa mawazo" na kuwa mwalimu bora. Kwa hivyo ingia darasani ukiwa na mtazamo chanya kuelekea wanafunzi wako, na tumia mifano rahisi na iliyo bora ili kumfanya mwanafunzi cijunze hili ndilo lengo kuu la uwepo wako shulen.

Teacher Talk

Usimamizi Bora wa Darasa

By: Mwalimu Michael K. Gitau
Star High School

Usimamizi bora wa darasa au uwezo wa kulimudu darasa ni utaratibu wa kuhakikisha darasa lipo katika hali bora ili kumwezesha mwalimu kufundisha kwa umahiri na wanafunzi kusoma au kujifunza kwa ufasaha.

Ili
wanafunzi
waweze
kujifunza
na
mwalimu
aweze



kufundisha, chumba cha darasa lazima kiwe kimeandaliwa vizuri na wanafunzi na mwalimu wanatakiwa wawe wamejitarisha akilizao na hisia zao ili somo liende vizuri.

Lengo kuu la kuwa darasani ni mwalimu kufundisha na wanafunzi kujifunza. Kwa hivyo ni muhimu kuzingatia hali nzuri ya darasa kwa mwalimu na mwanafunzi ili tendo la kufundisha na kujifunza yaweze kufanikiwa vyema.

M pangilio bora wa darasa katika nyanja za nidhamu, umakini na kukaza fikra kwa wanafunzi wanapo fundishwa unapelekea somo kufundishwa na kuelewaka vizuri.

Jinsi mwalimu anavyo pangilia darasa lake

anapaswa kufikiria mahitaji ya mwanafunzi ili mwanafunzi aweze kukazia fikra, kushiriki na kufanya majadiliano pamoja na wenzake. Kwa hivyo mpangilio wa darasa lolote ni lazima uwe rahisi na wenye kubadilika. Idadi ya wanafunzi na nafasi au ukubwa wa darasa ndivyo vinavyo toa mwongozo wa mpangilio wa darasa.

Nidhamu ya mwalimu na mwanafunzi ni sehemu au kiini muhimu cha kumfanya mwalimu alimudu darasa. Mwalimu anapo watia

nidhamu wanafunzi anatakiwa kulenga kubadilisha utovu wa nidhamu na kuhakikisha wanakuwa wanafunzi bora. Jambo la muhimu hatupaswi kuchanganya nidhamu na adhabu ambaye hulenga kurekebisha tabia kwani, kazi ya adhabu ni kudhibiti utovu wa nidhamu.

Njia kuu na bora yakumtia nidhamu mtoto ni ushauri nasaha. Ili ushauri uwe bora na wenye manufaa kwa mtoto ni lazima chanzo cha utovu wa nidhamu kijulikane. Kwa hiyo historia ya utovu wa nidhamu wa mwanafunzi inatakiwa kuhusihwa wakati wa ushauri nasaha. Kwa njia hii mtoto anawenza kubadili tabia yake mbaya, tofauti na adhabu ambayo ina mfanya ajihisi amenyanyasika na kutendewa isivyohaki, na kumsababisha ashindwe

Continued on page 7...

Psychosocial and Health


Kurejesha Watoto Waishio Mitaani Katika Malezi ya Familia



Shirika la TFT lilituma wawakulishi katika mkutano huu uliofanyika Dar es Salaam ijumaa ya tarehe 18 na 19 Novemba kuhuduria mafunzo mbalimbali kujua jinsi gani tunaweza kuwasaidia watoto waishio katika mazingira hatarishi. Mkutano huu ulikua na washiriki kutoka nchi 15 Ulimwenguni tukishirikishana uzoefu katika malezi bora ya watoto katika familia na kupunguza au ikibidi kuepukana kabisa na swala la watoto kukaa mitaani na kuijingiza kwenye mambo maovu.

Kongamano hili lilikuwa na manufaa makubwa sana kwetu kama walezi wa watoto katika jamii kubwa inayotuzunguka. Tulijifunza kujua na kujifunza kutoka kwa watoto. Kupenda kujua

kwanza kabisa mtoto anahitaji nini? Kwanini yuko jinsi alivyo? Nini hasa anachohitaji? Kuijua familia ya mtoto vizuri na kujenga urafiki na mtoto na familia kabla ya kufanya mipango ya kumrudisha katika familia. Tumejifunza kupitia mashirika mengine kazi wanazofanya na mafanikio waliyofikia katika malezi ya watoto pamoja na kuwaunganisha watoto na familia hata baada ya kukaa mbali na familia kwa miaka au miezi kadhaa.



Hatua za kushughulikia tatizo la mhusika katika kumuunganisha na familia

In Focus:

Cornerstone Leadership Academy

The Cornerstone Leadership Academy in Tanzania is an “Advanced Level” boarding high school. The students spend 2 years at the Academy before they go on to university. Since high school in Tanzania is for only two years, the school will take on 100 students in the school at a time. The school offers the national curriculum of Tanzania but with added emphasis on Leadership.



The School's Mission Statement:

We seek to create a life transforming learning environment that will mold young men and women into future leaders for

Tanzania... men and women whose lives fully reflect the character qualities and leadership principles embodied in the life of Jesus.

Our vision is to invest in young people who will become role models and leaders of high moral caliber so as to be a great positive influence on many others in the future. Our approach has proven its ability to instill in the African young people character qualities derived from basic, timeless and sound moral principles. We measure our success primarily in terms of changed lives. This is evidenced through criteria such as: exemplary behavior, compassion for others, trustworthiness, wise choices, willingness to work, a cooperative attitude and a sense of purpose in life. Also to learn to live together as brothers and sisters – as part of a



movement of men of integrity and women of virtue united under principles, precepts and person of Jesus. By this we are addressing the core issue behind all the conflicts in Africa.

Admission procedures

Every year few days after the release of O'level National Exam results between Feb and March we carry out a sequence of interviews, we later on admit 50 new students.

Adverts are made through different media so as to reach out to majority and a variety of other communication means are employed



Wanafunzi wa shule ya msingi Sinai wakiwa wanajibu maswali ya kutathmini mradi wa somo la Haiba na Michezo.



Washiriki wa shindano la uandishi wa insha na uchoraji kutoka kata ya Leguruki na Maruvangu wakiwa katika zoezi la uandishi wa insha.

Continued from page 5...

Shule zilizoshiriki katika huu mradi wa majaribio ni : Maji ya chai, Upendo Academy, Maua, Tanzania Adventist, Sylus Anderson, Chemchem, Leguruki, Sinai na Kimandafu.

Utekelezaji wa mradi huu uliwezeshwa na waalimu wa somo la Haiba, wakuu wa shule husika, maafisa elimu wa kata husika, Ofisi ya Afisa Elimu Wilaya ya Meru na Shirika la The Foundation for Tomorrow. Tuliweza kufanya mikutano mitatu na waalimu waliokuwa wakisimamia utekelezaji wa mradi huu, pia mikutano miwili na maafisa elimu kwa mwaka 2015/2016. Lengo la mikutano hii lilikua kutoa taarifa za maendeleo ya mradi, mafanikio, changamoto na njia za kutatua changamoto, pia kujadili mwendelezo wa mradi huu iwapo shirika litajitoa kwa lengo la kuongeza wigo maeneo mengine.

Mwezi Julai shirika liliendesa tathmini(Evaluation) ya mradi wa Haiba na michezo kwa shule 9. Shule 6 zikiwa zile zilizoshiriki na shule 3 zikiwa ni za majaribio ya kuweza kupima tofauti kati ya zile zilizopata mradi na zile ambazo hazikupata. Tathmini hii ilifanywa kwa

njia ya mahojiano, majadiliano na kujaza fomu. Walengwa waliohusika ni wakuu wa shule, waalimu wa somo la haiba, wanafunzi na viongozi toka ofisi za elimu almashauri ya Meru. Pindi ripoti yah ii tathmini itakapokamiliika tutawashirikisha wahusika wote.

Shule zilizohusika kwenye tathmini ni Chemchem, Sylus Anderson, Upendo , Maua, Sinai, Happy watoto, Amani, na Londeiya.

Kwa sasa Shirika la TFT limefunga mradi huu kwa shule zilizoshiriki, mradi utakua unaongozwa na shule husika, shirika litakuepo kwa ajili ya ushauri au msaada wa utekelezaji wa ufundishwaji wa Haiba. Dhumuni la shirika kujitoa kutoka asilimia 100% hadi 25 ni kwa ajili ya kupanua mradi huu kwa shule nyingine zenyehuitaji ambazo hazikufikiwa ndani ya halimashauri ya Meru.



Physical Address:
3rd Floor, King Solomon House
Anglican Church Compound
Old Moshi Road, Arusha
Tanzania

For comments/suggestions, email:
Noah@thefoundationfortomorrow.org
Or message/call: +255 753 661 770 / 684 468 774

Continued from page 6

so as to reach down to the grass roots societies too in the deep urban areas too.

The applicant will require the following at the first interview.

1. O'level results qualifying him/her to sit for Advanced Level Exams.
2. A short essay in the applicant's own handwriting giving his/her family history, personal and Leadership experience, goals and desired combination of study.
3. Two detailed reference letters from two people
- e.g. religious leaders, local leadership who can verify your potential, leadership experience, desirable character qualities, level of need, etc. ...
4. One letter from the Head teacher to verify that you were a student.
5. Two ID photos.
6. Personal ID either previous school, voters ID etc.
7. Birth certificate

Chemistry, Physics, Biology, Basic Applied Maths and General Studies.

In addition to the academic subjects, the student must be willing to participate fully in computer lessons and other sessions covering Inspirational Materials, Character Development, Leadership Principles and Social events.

For more information visit www.cornerstoneleadershipacademy.ac.tz or www.cornerstoneschoolsafrica.org

Classes offered for 2016

Academic subjects offered are History, Economics, Geography, English literature, Kiswahili, Mathematics,